**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA UFUNGUZI WA MAONESHO YA 48 YA KIMATAIFA YA BIASHARA YA DAR ES SALAAM, TAREHE 03 JULAI 2024 KATIKA UWANJA WA MAONESHO WA MWL. JULIUS NYERERE - DAR ES SALAAM**

- *Mheshimiwa Dkt. Eng. Filipe Jacinto Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji na Mgeni wetu Rasmi katika Maonesho ya 48 ya Kimataifa ya Biashara ya hapa Dar es Salaam;*

- *Mheshimiwa Omar Said Shaaban (MBW), Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar;*

- *Mheshimiwa January Makamba (Mb.), Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na ;*

- *Waheshimiwa Mawaziri wote mliopo hapa nasi;*

- *Mheshimiwa Manuel Jose Goncalves, Naibu Waziri wa Mambo*

*ya Nje na Ushirikiano wa Jamhuri ya Msumbiji;*

- *Mheshimiwa Ludovina Bernardo, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Viwanda na Biashara kule Msumbiji;*

- *Mheshimiwa Exaud Kigahe (Mb.), Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara na;*

- *Manaibu Mawaziri wote mlioko nasi hapa;*

- *Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mwenyekiti Kamati ya Bunge, Uchumi na Biashara;*

- *Mheshimiwa Albert Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mkuu wa Mkoa wa Manyara;*

- *Dkt. Hashil Abdallah, Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na ;*
- *Makatibu Wakuu wote na Naibu Makatibu Wakuu mliopo hapa, tunawashukuru sana kwa uwepo wenu;*

- *Viongozi wa Chama cha Mapinduzi na Viongozi wa Vyama vya Siasa ambao mko nasi hapa;*

- *Viongozi wa Dini;*

- *Prof. Ulingeta O.L. Mbamba, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya TanTrade pamoja na;*

- *Wajumbe wa Bodi natambua uwepo wenu;*

- *Bi. Latifa Mohamed Khamis, Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade;*

- *Viongozi wa Mashirika ya Umma na Binafsi;*

- *Menejimenti ya Wizara na Menejimenti ya TanTrade;*

- *Ndugu Washiriki wa Maonesho;*

- *Wageni Waalikwa;*

- *Wanahabari;*

- *Mabibi na Mabwana;*

***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!***

Nianze nami kumshukuru Mungu, pamoja na shukurani hizo kwa Mwenyezi Mungu, nitumie fursa hii kusema **vitu vitatu tu**.

**Kwanza kabisa**, kwa mimi mwenyewe na kwa niaba ya Serikali pamoja na Watanzania wote, nitumie fursa hii kumshukuru sana kaka na ndugu yetu, Mhe. Filipe Jacinto Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji, kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi kwenye Ufunguzi wa Maonesho haya ya mwaka huu. **Mhe. Rais ahsante sana.**

Niseme pia kwamba, uhusiano wa kibiashara kati ya watu wetu ulianza karne nyingi zilizopita kupitia mitandao ya kibiashara katika pwani yetu uliopelekea kuibuka kwa miji

mikubwa ya kibiashara kuanzia Mogadishu, kupitia Kilwa hadi Sofala, Msumbiji.

Ingawa urafiki ulianza enzi na enzi, ushirikiano rasmi kati yetu uliimarishwa zaidi na Waasisi wa Mataifa yetu mawili, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Hayati Sheikh Abeid Aman Karume kwa upande wa Tanzania na Hayati Eduardo Chivambo Mondlane na Hayati Samora Machel, kwa upande wa Msumbiji.

Jambo la kufurahisha ni kwamba, sisi viongozi tunaofuatia tumeendeleza dhamira hiyo ya kutaka kuimarisha ushirikiano kati ya Mataifa yetu; na ujio huu wa Mhe. Rais Nyusi hapa nchini na kwenye maonesho haya unadhihirisha dhamira hiyo. Hivyo, narudia tena kukushukuru sana Mheshimiwa Rais Nyusi kwa kukubali kuwa Mgeni Rasmi kwenye Maonesho haya.

**Suala la pili** ninalotaka kulisema ni kutoa shukrani na pongezi kwa waandaji wa Maonesho haya. Natambua shukrani na pongezi nyingi zimeshatolewa, lakini nami kama Mkuu wa Nchi nataka niongeze sauti yangu. Pongezi zangu za dhati kwa **Mhe. Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.),** ambaye nilimbadilisha kazi jana tu kabla ya leo, lakini natambua kazi kubwa aliyoifanya katika kutayarisha Maonesho haya, na kazi kubwa aliyoifanya katika kujenga Wizara ya Viwanda na Biashara. **Hongera zangu nyingi sana kwake.**

Aidha, naipongeza Bodi ya Wakurugenzi ya TanTrade chini ya Mwenyekiti wake **Prof. Ulingeta O.L. Mbamba,** Mkurugenzi Mkuu wa TanTrade **Bi. Latifa Mohamed Khamis,** Menejimenti na Wafanyakazi wote wa TanTrade kwa juhudi kubwa kuhakikisha Maonesho haya yanafanikiwa. Hakika tunajivunia

kazi yenu. **Hongereni sana.** Ni matarajio yangu kwamba mtaendelea kuboresha maonesho haya mwaka hadi mwaka, ili washiriki wanaokuja wavutiwe kurudi tena na tena.

*Ndugu zangu*, nimetaarifiwa kwamba, Maonesho haya yamefanikiwa kutokana na michango ya Wadhamini mbalimbali kutoka Taasisi za Umma na Binafsi. Kwa hili, niwashukuru wachache kwa niaba ya wengi waliojitokeza akiwemo **Bi. Cathy Wang – Mkurugenzi Mtendaji** wa Kituo cha Biashara cha Afrika Mashariki (EACLC), lakini Wadhamini Wakuu wa Maonesho haya ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, vilevile Shirika la Bima la Taifa (NIC) wadhamini wakubwa wa ndani ya Nchi, *Vodacom Tanzania kuwezesha Electronic gates* na ukataji wa tiketi kupitia Mtandao wa M-Pesa, na wengine wakiwemo TANESCO na TANROADS kama mlivyoona wamepewa zawadi hapa, kwa niaba ya Wadhamini wote, pokeeni shukrani zangu.

Ninawashukuru na kuwapongeza Viongozi na Washiriki wote kutoka sehemu mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kipekee, na hapa nasema kipekee, namshukuru na kumpongeza sana Mama Mkapa, na nimefurahi sana kumuona hapa. Mama Mkapa nilianza naye nikiwa afisa (*junior officer),* nikiwa kwenye banda lake la Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (*Equal Opportunity for All Trust Fund* – EOTF) wakati huohuo nikifanya kazi au nikiwajibika kama Jaji katika maonesho haya kwa miaka minne kutoka 1996 mpaka mwaka 2000. Ninashukuru nimeona banda la EOTF bado lipo na lipo imara, sikuingia ndani lakini nimepita nje. Kwa hiyo Mama Mkapa. **Hongera sana! Nakushukuru sana.**

***Mheshimiwa Mgeni Rasmi,***
***Ndugu Wananch, na***
***Washiriki wote wa Maonesho,***

**Suala la tatu** ninalotaka kulisema ni kuhusu kaulimbiu ya mwaka huu inayosema, ***'Tanzania, ni Mahali sahihi kwa biashara na uwekezaji'***.

Maonesho haya ya biashara ni nyenzo katika kuchochea maendeleo ya ukuaji wa sekta mbalimbali za kiuchumi. Tangu yaanze mwaka 1963 maonesho haya ya Sabasaba yamejizolea sifa nyingi barani Afrika na duniani kwa ujumla.

Ninafurahi kuwa, Maonesho ya mwaka huu yamekutanisha zaidi ya makampuni 3,486 kama yalivyochambuliwa hapa ya ndani na nje ya nchi. Hii inaonesha ukuaji na mvuto mkubwa ndani ya kanda na nje kwingineko kimataifa kwenye Maonesho haya ya biashara hapa Dar es Salaam.

Mvuto huu umechangiwa pia na juhudi za Serikali katika kusimamia misingi imara na thabiti katika kujenga uchumi

jumuishi na shindani kwenye nyanja mbalimbali ikiwemo Biashara, Viwanda na Uwekezaji. Ni ukweli usiopingika kuwa, njia mojawapo ya kufikia azma hii ni uendelezaji na uimarishaji wa ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa, na hivyo kufungua fursa mbalimbali za biashara na uwekezaji. Matunda ya kuimarika kwa ushirikiano tumeshaanza kuyaona. Mwaka 2023, Kituo cha Uwekezaji Tanzania kwa maana ya TIC kimesajili **miradi 504** mwaka jana yenye thamani ya Dola za Kimarekani **bilioni 5.68**. Hii ni kwa sababu watu wanakuja Tanzania, wanaona fursa, wanashiriki maonesho, wanatembelea mabanda mengine na kuona fursa zilizopo Tanzania na kuvutika kuja kuwekeza. Aidha, mauzo ya nje ya bidhaa zetu yalipanda kutoka **Shilingi Trilioni 12.3** mwaka 2019 hadi kufikia **Shilingi Trilioni 17.38** sawa na **Dola za Marekani Bilioni 6.57** mwaka jana 2023.

Niwahakikishie kuwa tunaendelea kujenga, kuboresha na kukamilisha miradi mbalimbali ya maendeleo ya miundombinu ili kuhakikisha tunaongeza tija kwa uzalishaji, kwa wingi na sifa *quality na standards.* Lakini vilevile, tuhakikishe kwamba tunakamilisha miradi ya miundombinu ili bidhaa zinazozalishwa ziweze kinasafirishwa kirahisi kufika kwenye masoko yanayokusudiwa. Vilevile, kazi hii tunayoifanya itaendelea kuwawezesha majirani zetu kunufaika kwa kutumia miundombinu hii katika kuchochea maendeleo ya ukuaji wa nchi zao. Ni kwa namna hii tutaendelea kuifanya Tanzania kuwa ***Mahali sahihi pa Biashara na Uwekezaji.***

Kwa msingi huo, nitoe wito kwa Watanzania wenzangu kutembelea na kushiriki Maonesho haya makubwa na kutumia vizuri programmu mbalimbali zinazoandaliwa katika kupata wadau wa biashara na uwekezaji.

Pia, nitoe rai kwa washiriki wote kutumia fursa hii vizuri kujifunza na kujipanga kuhudumia masoko makubwa ya ndani, kikanda na kimataifa. Bila shaka tumesikia kufunguka kwa Eneo Huru la Biashara la Afrika-AfCFTA, na hivyo niwaombe wale wote wenye bidhaa zenye viwango kufika TanTrade na kujisajili Wizara ya Viwanda na Biashara ili kunufaika na mpango huo. Nipongeze kampuni 11 ambazo zimeshaanza kutumia fursa hii muhimu kwa kusafirisha bidhaa za kahawa, katani, viungo, karanga na tumbaku kwenda nchi mbalimbali za Afrika ikiwemo Algeria, Nigeria, Misri, Ghana na Morocco. Nimesikia pia, baadhi yao wanashiriki maonesho haya na wapo katika Banda la Wizara ya Viwanda na Biashara ili kuhamasisha wengine kutumia fursa hiyo.

***Ndugu Wafanyabiashara,***

Serikali itaendelea kufanya kila linalowezekana kusikiliza na kutatua changamoto za wafanyabiashara nchini. Kwa mfanyabiashara yoyote mwenye maoni ya kuboresha, kujenga na kuisadia nchi, milango ipo wazi, waendelee kuwasiliana na Mamlaka zetu mbalimbali ikiwemo Wizara yenye dhamana ya Biashara bila kusahau Taasisi yake ya TanTrade.

Baada ya kusema hayo mambo matatu makubwa, kutoa shukrani, kutoa pongezi na maelezo kuhusu ukuzaji wa biashara na uwekezaji, sasa ninayo heshima ya kipekee kumkaribisha kaka yangu na ndugu yetu Mheshimiwa Filipe Jacinto Nyusi, Rais wa Jamhuri ya Msumbiji ambaye ni Mgeni Rasmi wa Maonesho haya ya 48 ya Biashara ya Kimataifa hapa Dar es Salaam ili aje kuhutubia na kisha kutufungulia rasmi maonesho ya mwaka huu 2024.

**Mheshimiwa Rais Karibu sana.**